



### Maswali

1. Huyo mtu alikuwa amefanyaje?
2. Mbona hakupenda kukaa na watu?
3. Mbona kulikuwa na tafaruku na umati wa watu?
4. Marafiki wa huyo mtu walitaka wafanye nini?
5. Mbona Yesu alitoa yule mtu kutoka kwa umati?
6. Yesu alifanyaje yule mtu?
7. Yesu alisema nini?
8. Nini ilifanyika kwa huyo mtu?
9. Yule mtu alisikia nini kwa mara ya kwanza?
10. Watu wote walisema nini?

### Majibu

1. Huyo mtu alikuwa kiziwi tena bubu.
2. Hakuelewa chenye watu walikuwa wakisema. Alionekana mjinga.
3. Kulikuwa na mtafaruku kwa sababu Yesu alikuwa amekuja.
4. Walitaka kumpeleka yule mtu kwa Yesu.
5. Kwa sababu yule mtu hakufurahia kuwa kwa umati wa watu.
6. Yesu aliweka vidole vyake ndani ya masikio ya yule mtu na kute ma mate na kuguza ulimi wake.
7. Yesu alisema, "Funguka."
8. Halafu aliweza kusikia na kuzungumza.
9. Alisikia maneno yenye watu walikuwa wakisema, ndege wakiimba hata upepo ukivuma kwa miti.
10. Watu walisema, "Ajabu! Yesu anafanya kila kitu vizuri."

## 42 Yesu anaponya mtu kiziwi tena bubu

### Marejeo

Marko 7: 32 – 37

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba kila mara Yesu alikuwa tayari kusaidia watu

### Maneno maalum

- 42.1 Kiziwi tena bubu + alitengwa na watu + hakusikia maneno ya Yesu
- 42.2 Umati + marafiki wa mtu + Yesu + tafadhali ponya + ondoa kwa umati
- 42.3 Yesu + vidole kwa masikio + tema + guza ulimi + "Funguka."
- 42.4 Alisikia na kuzungumza + umati + ajabu + Yesu anafanya kila kitu vizuri

**42.1** Hili somo ni juu ya Yesu vile aliponya mtu aliyejkuwa kiziwi tena bubu. Huyo kiziwi hakuweza kusikia kabisa. Tunajifunza kuzungumza kwa kuwasikiliza wazazi wetu. Huyu mtu alizaliwa kiziwi kwa hivyo hakuweza kuzungumza vizuri. Hakuweza kusikia wala hakuweza kuzungumza vizuri.

Huyu kiziwi tena bubu aliishi karibu na Bahari ya Galilaya. Hakuwa kwa watu wengine kwa sababu hakusikia walichosema. Wakati mwingine watu hawakumvumilia kwa sababu hakuwajibu walichomwambia. Hawakusikia alichojaribu kusema. Hii ilimfanya aonekane mjinga, kwa hivyo hakupenda kukaa na watu.

Labda huyu bubu alikuwa amemwona Yesu hapo awali. Lakini wakati wote kulikuwa na umati wa watu kwa hivyo hakuelewa maajabu yenye Yesu alikuwa akisema au kutenda. Ilikuwa vigumu sana na alikosa mambo mengi mazuri.

**42.2** Siku moja kulikuwa na mtafaruku Watu walikuwa wanakimbia kwa barabara. Watu waliendelea kuwa wengi mpaka hakukuwa na nafasi ya kutembelea. Huyo kiziwi tena bubu alitaka kwenda nyumbani. Hakupenda umati.

Marafiki wa huyo mtu walimpata. Walitaka wampeleke kwa Yesu. Walizukumana kwa umati watu. Baadaye walismama mbele ya mtu wa uso wa ukarimu wenye yule kiziwi tena bubu aliona kila siku. Marafiki walimuuliza Yesu aponye yule kiziwi tena bubu.

Yule bubu aliona hayo ni magumu tena ya kushangaza. Umati ulimpea huyu mtu uoga kwa sababu walikusanya karibu naye ili waone na kusikia kila kitu. Bubu aliangalia uso wa Yesu na akajua kwamba Yesu alimuuelewa. Yesu alirukisha macho yake juu ya yule mtu kuangalia huo umati wa watu na baadaye akamshika mkono, akamuongoza hatua kidogo kutoka kwa watu.

**42.3** Yesu akasubiri kidogo. Anawezaje kufanya huyu mtu aelewé chenyé atafanya? Atamfanya aelewé kwa vitendo. Kwa upole aliweka vidole vyake kwa masikio yake yaliyokuwa hayasikii. Akatema mate na kuguza ulimi wake usiokuwa ukizungumza. Yesu aliangalia mbinguni na kusema, "Funguka."



**42.4** Punde tu mtu huyu aliweza kusikia na kuzungumza vizuri. Baada ya miaka mingi aliweza kusikia watu wengine na kuzungumza nao. Angeweza kusikia ndege wakiimba na upopo ukivuma. Angesikia watu wakisema, "Ajabu! Ajabu! Yesu anafanya kila kitu vyema. Anaweza kufanya kiziwi asikie na bubu kuzungumza."

Yule mtu aliyejkuwa kiziwi tena bubu alitabasamu tu. Haya yalikuwa maneno ya kwanza yeye kusikia, na alijua kwamba ni ya kweli.